

**Swahili transcript:**

Tanzania ni muungano wa nchi mbili, ilikuwa ni nchi ya Tanganyika zamani, Tanganyika pamoja na Unguja, kwa hiyo zilipoungana, ndio ikazaliwa nchi ya Tanzania. Kwa hiyo kuna Tanzania bara na Tanzania visiwani, na Tanzania visiwani tunaiita Zanzibar. Kwa hiyo watalii wengi wanapoitembelea Tanzania, Tanzania bara, pia wanakwenda Zanzibar. Na Zanzibar imekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa watalii kwa sababu ni kisiwa. Kwa hiyo watalii wengi wanapenda kwenda Zanzibar, wanafurahi kukaa katika hoteli za kitalii kule, kuna mambo mengi ya kihistoria ambayo watalii wengi wanapenda kwenda kujifunza na kujionea wenyewe katika nchi ya Zanzibar. Kwa mfano ukichukulia aah! zamani ndipo lilipokuwa soko la watumwa wakati wa ukoloni, kwa hiyo watalii wengi wanapoitembelea Zanzibar pia wanakwenda Zanzibar kujionea mambo ya kihistoria kama soko la watumwa lililokuwa Zanzibar, na kuna vivutio vingine pia ambavyo viko katika Zanzibar, na wengi wanafurahia madhari nzuri ya nchi hii ya Zanzibar kwa sababu pia imezungukwa na bahari ya Hindi Kwa hiyo wanapata muda mzuri wa kupanda boti na kuzunguka na kujionea madhari nzuri ya nchi hii. Kwa hiyo tunajivunia watanzania kuwa na nchi hii nzuri ambayo ina mandhari nzuri kabisa kwa watanzania wenyewe na hata watalii ambao wanaitembelea Tanzania.

**English translation:**

Tanzania was formed after Tanganyika and Zanzibar were united. That is why we call it the United Republic of Tanzania. There is mainland Tanzania and the island of Tanzania, which we call Zanzibar. When visiting mainland Tanzania, many tourists also go to Zanzibar. They like to go there because it is an island, and they enjoy staying in tourist hotels. Moreover, they go to Zanzibar to learn some historical facts. As we know from the colonial era, there was a slave market in Zanzibar. Many tourists enjoy going and staying there for historical reasons. They also enjoy a good view of Zanzibar. The Indian Ocean surrounds the island, so they have a good time going out on boats for fun, and they

get a good view of Zanzibar. We Tanzanians are proud of having a fine country with many good views.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated